



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

Mji wa Serikali - Mtumba, Barabara ya Afya, S. L. P 573 - 40478 Dodoma.

Simu Na: 255(026)2963341/2963346, Nukushi: 255(026)2963348

Barua Pepe: [ps@jamii.go.tz](mailto:ps@jamii.go.tz), Tovuti: [www.jamii.go.tz](http://www.jamii.go.tz)

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **KUUNGANISHWA KWA VYUO VYA MAENDELEO YA JAMII, VYUO VYA MAENDELEO YA JAMII UFUNDI NA TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU**

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inautangazia umma kuwa, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) imefikia uamuzi wa kuviunganisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Vyuo vilivyounganishwa na Taasisi hiyo ni Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare (Mara), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha (Iringa), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba (Iringa), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli (Arusha), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole (Mbeya), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale (Ruvuma), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Mabughai (Tanga) na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi (Mwanza).

Kuanzia tarehe 04 Juni, 2026 Vyuo hivyo vimekuwa Kampasi za Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Uamuzi huo unalenga kuimarisha ufanisi wa kiutendaji na kuongeza ubora wa utoaji wa mafunzo ya taalauma ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, uamuzi huo ni mwendelezo wa juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuboresha upatikanaji wa wataalamu wa kada ya Maendeleo ya Jamii nchini ili kufikia malengo

ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, hususan katika eneo la kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii.

Wizara inawakaribisha wadau wa Maendeleo ya Jamii, vijana na wananchi wote wenye nia ya kujenga taaluma katika kada ya Maendeleo ya Jamii, kutumia fursa hiyo kujiunga na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kupitia Kampasi zake zilizopo katika maeneo mbalimbali nchini ili kupata ujuzi na maarifa bora katika kada ya Maendeleo ya Jamii.



Charles F. Komba

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**30 Juni, 2026**